**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI MKUU KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

---

*[Imetolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016]*

Ofisi ya Bunge
S.L.P 941
Dodoma

**APRILI, 2019**

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI MKUU KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020**

---

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa afya, uzima na nafasi nyingine ya kukutana hapa Dodoma katika Mkutano huu wa Kumi na Tano wa Bunge la Kumi na Moja.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 6 (2)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, kimeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria jukumu la kusimamia shughuli za Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu.

Aidha, Kanuni ya 7(1) (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 inatoa Mamlaka kwa Kamati zote za Kisekta kushughulikia bajeti za Wizara inazozisimamia. Jukumu hili la Uchambuzi wa Bajeti linaendana sambamba na jukumu la ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilifanya ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo nchini, iliyotengewa na kupokea fedha katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 kuanzia tarehe 12 hadi 19 Machi 2019. Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Bajeti za Wizara na Taasisi inazozisimamia kuanzia tarehe 21 hadi 27 Machi, 2019 ikiwemo Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira, Watu wenye Ulemavu na Uwekezaji ina Mafungu 6 ya bajeti kama ifuatavyo;

i) **Fungu 37** - Ofisi ya Waziri Mkuu,
ii) **Fungu 25** - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu,
iii) **Fungu 65** – Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu,
iv) **Fungu 15** - Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA),
v) **Fungu 61** - Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), na
vi) **Fungu 27** - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa Tanzania

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo Manne yafuatayo:-

i) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa Fedha unaoisha;
ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;
iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na;
iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

## 2.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Katiba na Sheria ilipokea taarifa ya utekelezaji wa **Mradi Na. 6581** wa Programu ya Kukuza Ujuzi nchini, ambao kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ulitengewa kiasi cha **Shilingi Bilioni Kumi na Tano (15,000,000,000/=).**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa na upatikanaji wa Fedha za kutekeleza Mradi huo, kwani kwa kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019 Ofisi ya Waziri Mkuu imepokea kiasi cha **Shilingi Bilioni Kumi na Mbili (12,000,000,000/) sawa na asilimia 80%** ya

Bajeti ya Mradi huo iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA OFISI YA WAZIRI MKUU KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa fedha 2019/2020, kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016, tarehe 21 hadi 22 Machi, 2019. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

### 3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ulitazama mlinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge Aprili 2018 na kiwango ambacho kimepokelewa kwa kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi 2019.

Aidha, uchambuzi huu ulitazama kiasi cha fedha kilichoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 na kiasi cha Fedha

kilichopokelewa katika Miradi ya Maendeleo hadi kufikia Mwezi Machi 2019. Lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu Mwelekeo wa Mpango na Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 ili kujua vipaumbele vya kibajeti.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati ulitazama pia eneo la ukusanyaji wa Maduhuli kwa kulinganisha kiasi kilichokusanywa katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi 2019 na ukamilishaji wa lengo la ukusanyaji lililowekwa wakati wa kupitisha bajeti Mwezi Aprili 2018. Lengo la uchambuzi wa namna hii ni kufahamu uwezo wa Serikali katika kukusanya Maduhuli. Kamati ilitumia njia mbalimbali katika uchambuzi wake kama kutazama hali halisi ya kila Taasisi, kujiridhisha na taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu kwenye Kamati.

## 3.2 Uchambuzi wa Taarifa Kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Bunge lako Tukufu liliidhinisha Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli yenye jumla ya **Shilingi Bilioni Thelathini na Tisa, Milioni Mia Nane Tisini na Nane na Thelathini Elfu, Mia Moja Themanini na Saba (39,898,030,187/=).** Katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Februari, 2019 kiasi cha Maduhuli kilichokusanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake ni **Shilingi Bilioni Kumi na Tisa, Milioni**

**Mia Mbili Tisini na Saba, Laki Sita Ishirini na Saba Elfu, na Mia Tisa Hamsini (19,297,627,950/=)** sawa na **asilimia 48** ya Makusanyo yaliyoidhinishwa na Bunge.

Aidha, Kamati imebaini kuwa, kwa Fungu 37 (Ofisi ya Waziri Mkuu) tayari imevuka malengo ya ukusanyaji wa Maduhuli kwa kufanya makusanyo ya **Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Moja Thelathini na Tisa, Laki Nne Ishirini na Saba Elfu, Mia Tisa Hamsini(1,139,427,950/) sawa na asilimia 114%** ya Makusanyo yaliyokusudiwa chini ya Fungu hilo.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, ongezeko hilo limetokana na hatua ya Serikali kufanyia kazi mapendekezo na Ushauri wa Kamati pamoja na Bunge lako Tukufu kuhusu kuboresha mitambo na utendaji wa Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Aidha, Ofisi hiyo imeongeza ufanisi katika makusanyo kiasi cha kuvuka lengo lililokusudiwa kwa Mwaka mzima ndani ya Robo Tatu ya Mwaka.

**Kamati, inaipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuwa mfano bora na wa kuigwa na Wizara pamoja na Taasisi zote za Serikali katika kuongeza ubunifu wa vyanzo vya mapato ya Serikali, hatua ambayo itasaidia kupunguza utegemezi kutoka nje ya nchi.**

3.3 **Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida kutoka Hazina**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Mafungu yanayosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Taasisi zilizo chini yake yalitengewa **Shilingi Bilioni Sitini na Sita, Milioni Mia Moja Sitini na Sita, Laki Tatu Themanini na Tisa Elfu, Mia Sita Tisini na Nane (66,166,389,698/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Kumi na Tisa, Milioni Mia Mbili, Laki Tano Sabini na Mbili Elfu, Mia Tano Tisini na Nne (19,200,572,594/=)** iliombwa na kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi Bilioni Ishirini na Tatu, Milioni Mia Moja Thelathini na Sita, Laki Tatu Hamsini na Moja Elfu na Hamsini na Tatu (23,136,351,053/=)** iliombwa na kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Matumizi mengineyo na **Shilingi Bilioni Ishirini na Tatu, Milioni Mia Nane Ishirini na Tisa, Laki Nne Sitini na Sita Elfu na Hamsini na Moja (23,829,466,051/=**) iliombwa na kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ruzuku kwa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Msajili wa Vyama vya Siasa.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Februari 2019 Taasisi hizo zilipokea **Shilingi Bilioni Thelathini na Saba, Milioni Mia Tano Ishirini na Nane na Ishirini na Nane Elfu, Mia Tatu Sabini na Saba (37,528,028,377/=)** sawa na **asilimia 58%** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge**.** Uchambuzi wa uwiano wa Bajeti iliyoidhinishwa na upatikanaji wa fedha ya Matumizi

ya Kawaida hadi kufikia Februari 2019 umeainishwa katika **Jedwali Na. 1** .

**JEDWALI NA. 1: Uchambuzi wa Uwiano wa Bajeti iliyoidhinishwa na Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida hadi kufikia Februari, 2019**

| **NA.** | **FUNGU** | **BAJETI ILIYOIDHINISHWA** | **FEDHA ILIYOPATIKANA** | **ASILIMIA** |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 37-OFisi ya Waziri Mkuu | 17, 427,714,000 | 7,834,885,500 | 45 |
| 2 | 25 - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu | 7,016,012,000 | 4,835,194,549 | 69 |
| 3 | 65 – Kazi, Ajira ,Vijana na Wenye Ulemavu | 13,644,067,698 | 7,751,904,840 | 57 |
| 4 | 27- Msajili wa Vyama vya Siasa | 19,409,941,000 | 12,736,816,350 | 66 |
| 5 | 15-Tume ya Usuluhishi na Uamuzi | 3,828,024,000 | 1,983,154,547 | 52 |
| 6 | 61- Tume ya Taifa ya Uchaguzi | 4,840,631,000 | 1,959,814,168 | 41 |
| | **JUMLA** | **66, 166,389,698** | **37,528,028,377** | **58** |

**Chanzo: Taarifa ya WN-OWM, tarehe 21 Machi, 2019**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi huu unaonyesha kuwa kumekuwa na mwenendo mzuri kuhusu upatikanaji wa fedha kwa kila Fungu.

**Mheshimiwa Spika,** Maoni ya Kamati ni kwamba hali ya upatikanaji wa fedha kwa wakati inatakiwa kuendelea na kuzingatiwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, ili kurahisisha usimamizi na Utekelezaji wa Shughuli mbalimbali za Serikali kwa wakati na kwa ufanisi.

## 3.4 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019,

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Ofisi ya Waziri Mkuu iliidhinishiwa Fedha za Miradi ya Maendeleo kiasi cha **Shilingi Bilioni Hamsini na Nane, Milioni Mia Saba Tisini na Moja, Laki Nne Arobaini na Moja Elfu (58,791, 441,000/=)** kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni Thelathini na Moja (31,000,000,000/=)** ni fedha za ndani na **Shilingi Bilioni Ishirini na Saba, Milioni Mia Saba Tisini na Moja, Laki Nne Arobaini na Moja Elfu (27,791,441,000/=)** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** hadi Februari, 2019 Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizopokelewa ni **Shilingi Bilioni Thelathini na Sita, Milioni Mia Tisa Sabini na Mbili, Laki Tisa Themanini na Tano**

**Elfu, Mia Saba Themanini na Tisa (36,972,985,789/=) sawa na asilimia 63%** ya Fedha iliyoidhinishwa na Bunge.

## 3.5 Yatokanayo na Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa upatikanaji wa Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kwa robo tatu ya Mwaka wa Fedha 2018/2019 siyo wa kuridhisha kwa kuwa, Mfuko huo haujapokea kiasi chochote cha Fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Maoni ya Kamati ni kuwa, pamoja na Vijana kuendelea kunufaika na Mikopo mbalimbali kupitia Halmashauri nchini, bado kuna kila sababu kwa Serikali kutoa fedha za Mfuko wa Manedeleo ya Vijana kabla ya kuisha kwa Mwaka huu wa Bajeti 2018/2019.

# 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kuchambua Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 tarehe 21 hadi 22 Machi 2019. Mpango huu na Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 umeandaliwa kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 - 2020, Mwongozo wa Mpango wa

Bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mpango ambao umelenga utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17-2020/2021).

## 4.1 **Uchambuzi wa Vipaumbele vya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu**

**Mheshimiwa Spika,** Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 umeainisha maeneo 29 ya vipaumbele yakiwemo;

i) Kuchapa Nyaraka mbalimbali za Uendeshaji wa Shughuli za Serikali Kuu, Bunge na Serikali za Mitaa,
ii) Kujenga uwezo wa Serikali kukabiliana na Maafa;
iii) Kuratibu na kusimamia Maendeleo ya Uwekezaji Nchini,
iv) Kuratibu na kusimamia Shughuli za Baraza la Taifa la Biashara,
v) Kuratibu Shughuli za Bunge na kushughulikia kero na malalamiko ya Wananchi;
vi) Kusuluhisha Migogoro sehemu za Kazi,
vii) Kuratibu na kusimamia uwezeshaji wa Maendeleo ya Vijana,
viii) Kuratibu na Kusimamia Masuala ya Fidia kwa Wafanyakazi wanaoumia, kufariki au kupata madhara ya kiafya wakiwa kazini,
ix) Kuratibu Utekelezaji wa Sera, Sheria na Mikakati ya Kukuza Ajira nchini na kuongeza nafasi za Ajira za Watanzania nchi za nje,

x) Kusimamia, Kuratibu na kutoa huduma kwa Watu wenye Ulemavu, na
xi) Kuratibu Maadhimisho na Sherehe za Kitaifa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliridhishwa na vipaumbele viliyowekwa na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu vinaendana na Mpango wa Taifa wa Mwaka 2019/2020. Aidha, Kamati imeridhika na vipaumbele hivi kwa sababu vinajumuisha maeneo yote ya msingi ambayo yapo katika Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana, Watu wenye Ulemavu na Uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika**, **pamoja na vipaumbele hivyo Kamati inatoa rai kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha kwamba vipaumbele vyake vinalenga kuboresha na kuimarisha mazingira wezeshi ya uwekezaji kwa lengo la kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi, hatua ambayo itatengeneza Ajira kwa Wananchi wengi na kuongeza fursa mbalimbali za biashara na mapato kwa Wananchi na Taifa kwa ujumla hivyo, kupunguza utegemezi mkubwa wa kibajeti kutoka nje ya Nchi.**

## 4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Ofisi ya Waziri Mkuu inatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi Bilioni Arobaini, Milioni Mia Tisa Kumi na Tatu, Laki Moja Hamsini na Nne Elfu, Mia Mbili (40,913,154,200/=).** Makadirio ya Makusanyo yanaongezeka kwa **Shilingi Bilioni Moja na Milioni Kumi na Tano, Laki Moja Ishirini na Nne Elfu na Kumi na Tatu (1,015,124,013/=),** ongezeko hilo ni **sawa na asilimia 2.5%** ya Bajeti ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na Mpango wa Ofisi ya Waziri Mkuu wa kuongeza Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, kwa kuwa Ofisi hiyo imedhihirisha uwezo na ubunifu mkubwa katika ukusanyaji wa Maduhuli kiasi cha kuvuka lengo ndani ya Robo tatu ya Mwaka wa Fedha 2018/2019.**

**Mheshimiwa Spika,** Maduhuli haya yatakusanywa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu **(Fungu 37),** Tume ya Taifa ya Uchaguzi (**Fungu 61),** Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, **(Fungu 65)** na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa (**Fungu 27).** Sehemu kubwa ya Makadirio ya Maduhuli haya yatatokana na shughuli za Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali katika kuchapa Nyaraka mbalimbali za Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, pamoja na Nyaraka za matukio maalumu. Sehemu nyingine inayotegemewa kutoa Maduhuli

zaidi ni **Fungu 65** ambalo linahusisha Taasisi mbalimbali zilizo katika Sekta ya Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu.

**Mheshimiwa Spika**, mchanganuo wa kiasi cha Maduhuli kinachotegemewa kukusanywa kwa kila Fungu ni kama ilivyoainishwa katika Jedwali **Na.2.**

**Jedwali Na.2. Makisio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, Ofisi ya Waziri Mkuu**

| FUNGU | TAASISI HUSIKA | MADUHULI YALIYOIDHINISHWA 2018/2019 | MAKADIRIO YA MADUHULI 2019/2020 |
|---|---|---|---|
| 27 | Msajili wa Vyama vya Siasa | 175,000 | 10,300,000 |
| 37 | Ofisi ya Waziri Mkuu | 1,000,000,000 | 2,000,000,000 |
| 61 | Tume ya Taifa ya Uchaguzi | 15,000,000 | 20,000,000 |
| 65 | Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu | 38,882,855,187 | 38,882,854,200 |
| **JUMLA** | | **39,898,030, 187** | **40,913,154,200** |

## 4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Ofisi ya Waziri Mkuu inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi Bilioni Sabini na Tano, Milioni Mia Nane Themanini na Nne, Laki Tisa Sabini na Nane Elfu (75,884,978,000/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi Mengineyo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Kumi na Nane, Milioni Mia Nane Themanini na Moja, Laki Nne Tisini na Tano Elfu, Mia Nne Tisini na Tisa (18,881,495,499/=)** ni kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi Bilioni Thelathini, Milioni Mia Saba na Mbili, Laki Nane Thelathini na Tano Elfu, Mia Tisa Arobaini na Nane (30,702,835,948/=)** ni Ruzuku kwa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Msajili wa Vyama vya Siasa na **Shilingi Bilioni Ishirini na Sita, Milioni Mia Tatu, Laki Sita Arobaini na Tano Elfu, Mia Saba Hamsini na Moja (26,300,645,751/=**) ni fedha za Matumizi Mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake imeongezeka kwa kiasi cha **Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Saba Kumi na Nane, Laki Tano Themanini na Nane Elfu, Mia Tatu na Mbili (9,718,588,302/=) sawa na asilimia 14.7%** ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika,** ongezeko la Bajeti ya Matumizi ya Kawaida inatokana na sababu za msingi ikiwemo kuongezeka kwa Masuala ya Uwekezaji ili kukidhi mahitaji ya Muundo Mpya kutokana na Mabadiliko yaliyofanywa na Mheshimiwa Rais kwa kuongeza shughuli za Uwekezaji chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Aidha, kuanzishwa kwa Kitengo kipya cha Uratibu wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu ni mojawapo ya sababu ya ongezeko la Bajeti ya Matumizi ya Kawaida chini ya Ofisi hii.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaishukuru na kuipongeza Serikali, kwa kutekeleza ushauri na mapendekezo ya Kamati pamoja na Bunge lako Tukufu kwa kuanzisha Kitengo kipya cha uratibu wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu na kukitengea Kasima yake ya Kibajeti chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Hii ni pamoja na kuanza kazi kwa Baraza la Watu wenye Ulemavu kufuatia uteuzi wa Wajumbe wa Baraza hilo.**

**Mheshimiwa Spika, hatua hiyo inadhihirisha usikivu, utayari na dhamira njema ya Serikali katika kutatua changamoto mbalimbali za makundi Maalum ya Kijamii kwa Maendeleo Endelevu ya Makundi hayo.**

## 4.4 Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake zimeombewa **Shilingi Bilioni Hamsini na Sita, Milioni Mia Sita Thelathini na Tisa, Laki Tano Thelathini na Tatu Elfu, Mia Sita Thelathini na Saba (56,639,533,637/=)** kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni Kumi na Tisa (19,000,000,000/=)** ni fedha za ndani na **Shilingi Bilioni Thelathini na Saba, Milioni Mia Sita Thelathini na Tisa, Laki Tano Thelathini na Tatu Elfu, Mia Sita Thelathini na Saba (37,639,533,637/=)** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Bajeti ya Maendeleo inayoombwa imepungua kwa kiasi cha **Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Moja Hamsini na Moja, Laki Tisa na Saba Elfu, Mia Tatu Sitini na Saba (2,151,907,363/=)**. Pungufu hiyo ni sawa na **asilimia 3.7%** ya Bajeti ya Maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, mabadiliko hayo katika Bajeti ya maendeleo pamoja na sababu nyingine muhimu, yanatokana na kukamilika kwa kiasi kikubwa Ujenzi wa Makazi ya Waziri Mkuu, hapa Dodoma.

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Ofisi ya Waziri Mkuu katika Miradi ya Maendeleo katika Mwaka huu wa Fedha umelenga katika **maeneo Matano (5)** yakiwemo:-

i) Kutoa Mafunzo ya Kukuza Ujuzi kwa Vijana ili kuwawezesha kuwa na ujuzi wa kushiriki katika ujenzi wa Viwanda na kufikia uchumi wa kipato cha kati,
ii) Kuwawezesha Vijana Kiuchumi kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana,
iii) Kuwajengea uwezo wakulima ili kuyafikia masoko yenye tija ikiwemo masoko ya mitaji na pembejeo,
iv) Kuongeza uwezo wa kujiandaa na kukabiliana na maafa nchini, na,
v) Kujenga Mifumo ya utoaji taarifa za hali ya hewa na tahadhari za dharura iliyoboreshwa hapa nchini.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** ninaomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu masuala mbalimbali yaliyojitokeza katika uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake. Aidha, Maoni na Ushauri wa Kamati umezingatia pia Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2018/2019.

## 5.1 FUNGU 37- Ofisi ya Waziri Mkuu

i) **Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa na Kamati kwa Ofisi ya Waziri Mkuu katika Mwaka wa Fedha 2018/2019. Aidha, Kamati imeridhishwa na uwezo wa Ofisi hii katika kuongeza makusanyo ya Maduhuli kwa mwaka wa Fedha 2018/2019 kwa lengo la kupunguza utegemezi, hivyo, Serikali iendelee na jitihada hizo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

ii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuboresha Miundombinu ya kazi katika Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, hatua ambayo itaongeza Makusanyo ya Serikali. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuboresha Ofisi hiyo ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya kazi kwa Wafanyakazi wake. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa fedha zote zinazoombwa na kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii muhimu zinatolewa kwa wakati ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa haraka na kwa ufanisi.

iii) **Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuendeleza jitihada zake za kuhakikisha inapunguza kwa kiasi kikubwa utegemezi wa Fedha za Nje katika Miradi ya Maendeleo. Hatua hiyo inawezekana kama Serikali itaendelea kuongeza vyanzo vipya vya Mapato, kuboresha mazingira ya Uwekezaji nchini kwa kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuongeza kasi ya Ujenzi na Uendelezaji wa Viwanda nchini, hatua ambayo itaongeza fursa za kiuchumi na kuongeza pato la ndani.

iv) **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Waziri Mkuu ihakikishe inaimarisha Usimamizi wa Masuala ya Uwekezaji nchini kwa lengo la kuongeza na kuchochea ukuaji wa Uchumi wa Viwanda nchini kuelekea Uchumi wa Kati ifikapo mwaka 2025.

## 5.2 Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa

i) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa iendelee kuchunguza na kufuatilia mienendo ya Vyama vya Siasa, kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na weledi katika usimamizi na udhibiti wa mienendo ya Vyama vya Siasa ikiwemo kuchukua hatua stahiki kwa kila Chama kinachovunja Misingi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Sheria zingine za nchi, kwa lengo la kulinda Umoja, Udugu, Amani, Ulinzi na Usalama wa nchi kupitia mienendo ya Vyama vya Siasa.

5.3 **Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF)**

i) **Mheshimiwa Spika,** pamoja na Kamati kuridhishwa na kazi nzuri inayofanywa chini ya Mfuko huu, Kamati inashauri Mfuko uendelee kutoa Elimu ya kutosha kwa Waajili na Wafanyakazi hususan Vyama vya Wafanyakazi kwa lengo la kuhakikisha kuwa Waajili wote nchini wanazingatia matakwa ya Sheria katika kuhakikisha Wanajiandikisha kwenye Mfuko, wanalipa Ada/Michango stahiki kwa wakati na kutoa taarifa sahihi.

ii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kushauri Mfuko kuweka na kuimarisha Mfumo mzuri wa kufanya tathmini za fidia kwa Wafanyakazi wanaopata ajali kazini na kuhakikisha kwamba malipo ya fidia yanafanyika kwa haraka kwa kila Mfanyakazi aliyetimiza vigezo vya fidia.

5.4 **FUNGU 65 - Kazi na Ajira**

i) **Mheshimiwa Spika**, pamoja na Kamati kuridhishwa na utendaji kazi wa Mamlaka ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), Kamati inaendelea kushauri kuwa, OSHA iendelee kubuni mikakati endelevu na kuitekeleza kuhusu kusimamia Afya na Usalama wa Wafanyakazi Mahali Pa Kazi kwa kuzingatia ongezeko la uanzishwaji wa Viwanda nchini katika kulinda usalama wa Wafanyakazi.

ii) **Mheshimiwa Spika,** pamoja na Kamati kuridhishwa na hatua ya Serikali ya kuanzisha Kitengo cha kuratibu masuala ya Watu wenye Ulemavu nchini ikiwemo kuanzisha Rasmi Baraza la Taifa la kuratibu Masuala ya Kundi hilo kwa ujumla, Kamati inashauri kuwa, Ofisi ya Waziri Mkuu ihakikishe inasimamia kitengo hicho na Baraza husika ili vyombo hivyo vitekeleze majukumu yake

kwa weledi mkubwa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wanatatua migogoro mbalimbali inayoendelea katika Vyama vya Watu wenye Ulemavu nchini. Aidha, Mikopo inayotolewa na Halmashari kwa ajili ya Makundi hayo irejeshwe bila riba na Serikali isimamie na kudhibiti utoaji wa fedha hizo ili ziwafikie walengwa kwa wakati.

iii) **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-Tamisemi, wahakikishe wanaongeza udhibiti wa marejesho ya Mikopo ya Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ili Mfuko huo uwafikie Vijana wengi zaidi. Hatua hiyo iende sambamba na utoaji wa Elimu kuhusu matumizi bora ya fedha za Mfuko kwa maendeleo yaliyokusudiwa.

iv) **Mheshimiwa Spika,** Kamati inapongeza jitihada za Serikali katika kuwajengea ujuzi Vijana na makundi mbalimbali ya kijamii kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwemo mafunzo ya matumizi ya Shamba Kitalu katika maeneo mbalimbali nchini, kwa ajili ya kuyawezesha makundi husika kuhusu kilimo chenye tija. Hata hivyo, Kamati inashauri, kuwepo ushirikishwaji wa Wabunge wanaotoka kwenye Halmashauri husika kabla ya Serikali kuanzisha Miradi husika kwa lengo la kupanua ushiriki wa Vijana wengi waliokusudiwa kupitia wawakilishi wao ambao ni Wabunge.

## 5.5 FUNGU 61-Tume ya Taifa ya Uchaguzi

i) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kuishauri Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuboresha Daftari la Wapiga Kura na kuchukua jitihada za kutosha kwa uangalifu mkubwa katika uboreshaji wa Daftari hilo. Hatua hizi zijumuishe utoaji Elimu ya Uraia hususan uandikishaji wa Wapiga Kura Vijana wengi zaidi ili waweze kutumia haki yao ya Kikatiba ya kupiga au kupigiwa

kura. Hali hii itaongeza idadi ya Watanzania wengi zaidi watakaokuwa na sifa na vigezo vya kupiga kura katika chaguzi mbalimbali zinazokuja.

ii) **Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kuishauri Tume ya Taifa ya Uchaguzi kujitahidi kufanya kazi yake kwa Weledi ili kuendelea kuaminika kwa Wadau wake wa Uchaguzi. Hii ni pamoja na kuhakikisha kwamba, inawashirikisha Wadau wa Uchaguzi wakati wa uhuishaji wa Daftari la Wapiga kura ili kuepuka migogoro isiyokuwa na tija kwa Taifa.

iii) **Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kushauri kwamba, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ihakikishe inafuatilia wasimamizi wake wa Uchaguzi na kuwawajibisha pale wanapofanya uzembe unaosababisha madhara ambayo yangeweza kudhibitiwa mapema na msimamizi aliye makini na anayetambua na kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Sheria.

iv) **Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inatoa Fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa Wakati ili kuiwezesha Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuratibu masuala mbalimbali ya Uchaguzi kwa ufanisi Mkubwa.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukupongeza kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili vema na kwa weledi na umahiri wa hali ya juu. Nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza Naibu Spika Mheshimiwa Tulia Ackson, Mb, kwa weledi na umahiri wake katika kukusaidia kuongoza Bunge. Niwapongeze pia Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukushauri na kukusaidia kuendesha vikao vya Bunge. Wote kwa pamoja tunawaombea afya na uzima katika kutekeleza majukumu mliyopewa.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana, na Watu wenye Ulemavu, Mhe. Jenista J. Mhagama, (Mb), Waziri wa Nchi (Uwekezaji), Mhe. Angellah Kairuki, (Mb), Manaibu Waziri, Mhe. Antony Mavunde, (Mb), na Mhe.Stella Alex Ikupa, (Mb), Makatibu Wakuu na Wataalam wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao mizuri wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana,Watu wenye Ulemavu na Uwekezaji. **Naomba majina yao kama yalivyo katika Taarifa hii yaingie katika Taarifa Rasmi ya Bunge (Hansard):-**

1. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb – M**akamu /Mwenyekiti**

3. Mhe.Joseph Kizito Mhagama, Mb-Mjumbe;
4. Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb - Mjumbe;
5. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe;
6. Mhe. Amina Saleh Mollel, Mb - Mjumbe;
7. Mhe. Wanu Hafidh Amer, Mb - Mjumbe;
8. Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe, Mb - Mjumbe;
9. Mhe. Dkt. Mathayo David Mathayo, Mb - Mjumbe;
10. Mhe. Nimrod Elirehemah Mkono, Mb - Mjumbe;
11. Mhe. Susan Peter Maselle, MB - Mjumbe;-
12. Mhe. Alfredina Apilinary Kahigi, Mb - Mjumbe;
13. Mhe. Latifah Hassan Chande,Mb - Mjumbe;
14. Mhe. Ally Abdulla Saleh, Mb - Mjumbe;
15. Mhe. Jacqueline Kandidus Ngonyani Msongozi,Mb-Mjumbe;
16. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb - Mjumbe;
17. Mhe. Sixtus Raphael Mapunda, Mb - Mjumbe;
18. Mhe. Hassan Seleman Kaunje, Mb - Mjumbe;
19. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb - Mjumbe;
20. Mhe. Upendo Furaha Peneza, Mb – Mjumbe,
21. Mhe. Tundu Antiphas Mughwai Lissu, Mb - Mjumbe
22 Mhe. Emmanuel A.Mwakasaka, Mb - Mjumbe
23 Mhe. Dkt.Suzan Alphonce Kolimba, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, mwisho, kabisa lakini si kwa umuhimu napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, **Ndg. Stephen Kagaigai** kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, napenda kumshukuru

Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Angelina L. Sanga, Katibu wa Kamati hii, Ndg. Stanslaus Kagisa, na Msaidizi wa Kamati Ndg. Raheli Masima kwa kuihudumia vyema Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati. Napenda kuwashukuru Makatibu Muhtasi wa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuchapa taarifa hii. Napenda pia kuwashukuru Watendaji wote wa kitengo cha Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kwa kuhakikisha kwamba Taarifa hii inatoka kwa wakati na kwa ubora.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Kazi, Ajira, Vijana, Watu wenye Ulemavu na Uwekezaji, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii.

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb.
**MWENYEKITI,**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA**

4 Aprili, 2019